**الوفاء وحفظ الجميل**

# UTEKELEZAJI WEMA NA KULINDA MAZURI.

## “KHUTUBA YA KWANZA”

**Imefasiriwa na**

**Profesa.Ayman Alasar**

Shukrani zote ni Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote Mwenye kuzungumza kwenye Kitabu chake Kitukufu: {**Wala musisahau mazuri muyafanyayo kati yenu**} Ninashuhudia kuwa hakuna Mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Muhammd ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehema na amani kwake Mtume Muhammad pamoja na watu wake na Maswahaba zake na wale wote wanaowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi**:

Hakika kufanya wema na kuhifadhi uzuri ni miongoni mwa misingi ya ubinadamu na ni maadili mema ambayo yamelinganiwa na dini yetu ya kweli, kwani Mwenyezi Mungu amewasifu Manabii A.S kwa kusifika kwao na tabia hii nzuri, ambapo Mola Mtukufu Anasema kuhusu Mtume Ibrahimu A.S: {**Na Ibrahimu ambaye ametekeleza ahadi**} na Anasema Mola Mtukufu kuhusu Nabii Yahya AS: {**Na akawa mwema kwa wazazi wake, wala hakuwa mwenye kufanya maasi**}.

Hakuna shaka kuwa watu bora wa kufanyiwa wema na kuhifadhi uzuri wao ni wazazi wawili, kwani wao ndio watu bora kwa watoto wao, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameamrisha kufanyiwa wema wazazi wawili, ambapo Anasema Mola Mtukufu akiwakumbusha watoto kufanya mazuri kwa wazazi wao baada ya wazazi kufikia hatua ya utu uzima na kuanza kudhoofika: {**Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Nasema nao kwa kwa kauli ya heshima * Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Wafanyie huruma kama wao**

**walivyonifanyia huruma wakati wa kunilea kwao utotoni**}, kama vile kuwatendea mema wazazi kunaendelea hata baada ya kufa kwao ambapo Mtume S.A.W anasema: "*Hakika wema kwa mtenda wema ni mtoto kuendeleza wema kwa watu waliokuwa na upendo kwa baba yake*".

Miongoni mwa sura nzuri zaidi ya utekelezaji wema ni kufanya wema kati ya wana ndoa wawili kwa maana ya mume na mke, kwa kutekeleza haki, kuishi vizuri, kufanya wema ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: {**Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri**} na amesema Mtume S.A.W "*Wausieni wanawake mambo mazuri*", mwenye kuzingatia maisha ya Mtume wetu S.A.W ataona alikuwa ni mwema kwa mke wake Bibi Khadija R.A na kulinda uzuri wake katika kuliwaza kwake Bi Khadija na kumtetea kwake Mtume S.A.W, kwani Mtume S.A.W alikuwa mwema katika kumtaja kwake hata baada ya kifo chake, alikuwa anamsifu sana na kumuombea sana msamaha kwa Mwenyezi Mungu pamoja na kuwakirimu wale marafiki wa marehemu mke wake, ambapo alikuja mzee mmoja kwa Mtume S.A.W kisha Mtume alimpokea vizuri na kumkirimu, ndipo Bi Aisha alipouliza hilo na Mtume akamjibu: "*Huyu bibi alikuwa anakuja kwetu wakati wa uhai wa Bi Khadija na hakika kutekeleza wema ni katika imani*".

Na katika sura za wema ni pamoja na kufanya wema kwa watu wema, na hilo linaonekana wazi katika msimamo wa Mtume S.A.W pale alipowafanyia mazuri watu wa Madina ambao walimtetea baada ya kugawa mali za ngawira siku ya vita vya Hunain akisema kuwaambia: "*….Ninaapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad ipo mikononi mwake, lau isingekuwa hii kuhama basi ningekuwa ni miongoni mwa watu wa Madina, lau watu watapita makundi na watu wa Madina wakapita makundi basi ningelifuata kundi la watu wa Madina, Ewe Mwenyezi Mungu warehemu watu wa Madina na watoto wa watu wa Madina na watoto wa watoto wa watu wa Madina*", na akasema Mtume S.A.W kwa upande wao "*Hakika watu wa Madina wamemaliza waliyokuwa nayo, na yamebakia yenu, hivyo fanyeni wema kwa wafanya wema na jiepusheni na waovu*", na alikuwa

Mtume S.A.W anasema kumwambia Abibakri R.A. "*Hakika katika watu watoaji zaidi kwangu kwa ukaribu wake na mali zake ni Abubakri*".

Bali tabia ya wema kwa watu wema inakusanya mpaka watu wakiukaji, kwa kulinda uzuri wao, na hilo linaonekana wazi pale Mtume wetu S.A.W siku ya badri alipomtaja Mutwimu Ibn Adiyy, huyo mtu aliingia pamoja na Mtume Makka baada ya kurudi safari ya Twaif, anasema Mtume S.A.W "*Lau angelikuwa Mutwiim Ibn Adiyy bado yupo hai kisha akaniambia kuhusu hawa basi ningeliwaacha kwake*" anakusudia mateka wa vita vya badri.

Miongoni mwa sura za wema na kulinda mazuri ya mtu, ni kumfanyia wema mwalimu na wema huo ni kwa kumuheshimu na kumuombea duwa, anasema Abu Hanifa: Sijaswali tokea kufariki kwa Sheikh wangu Hamada isipokuwa namuombea duwa yeye pamoja wazazi wangu, na hakika mimi nitamuombea duwa kwa kile yule niliyejifunza kwake elimu au nimemfundisha elimu, na anasema Imamu Ahmad: Sijalala tokea miaka thelathini isipokuwa huwa ninamuombea duwa Imamu Shaafy na kumtakiwa msamaha.

********

## "KHUTUBA YA PILI"

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, swala na salamu zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wake na Maswahaba zake wote.

Hakika miongoni mwa sura za wema na kulinda mauzuri: Ni kufanya wema kwa ajili ya nchi, hakuna shaka hilo ni katika mambo ya watu wenye murua na wema, anasema Al-Aswmaii: Pindi unapotaka kufahamu wema wa mtu na utekelezaji wake basi angalia wema wake kwa nchi yake, mapenzi yake kwa ndugu zake, na hilo lipo wazi pale Mtume S.A.W aliposimama usiku wa kuhama Mjji wa Makka, na akauangalia Mji huo baaad ya watu kumfanyia kero na maudhi pamoja na Maswahaba zake na kumkadhibisha kwao akasema: "*Hakika yako Makka ni ardhi ipendwayo sana na Mwenyezi Mungu, lau watu wangu wasingenitoa kwako basi*

*nisingetoka*" na pindi alipoomba duwa Mtume S.A.W akiwa Madina alisema: "*Ewe Mwenyezi Mungu tupe upendo kwa Mji wa Madina kama vile ulivyotupa upendo kwa Mji wa Makka au zaidi*".

Hivyo hakuna ubaya kujipamba na tabia ya wema na kulinda mazuri, kwani yenyewe ni tabia nzuri kwa tabia hiyo huinua nafsi, na kukamilisha imani, ambapo Mtume S.A.W anasema: "*Mbora wa wafanyao wema ni wenye tabia nzuri*", na anasema Mtume S.A.W "*Hakika Waumini wakamilifu wa Imani ni wale wenye tabia njema zaidi*".

**Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba utuongoze kwenye tabia nzuri na uilinde Misri yetu na nchi zengine za ulimwengu wa Kiarabu na Kiislamu.**